


TaCRI

TAASISI YA UTAFITI WA KAHAWA TANZANIA

# Taarifa Ya Mwaka 2004

# YALIYOMO


UJUMBE WA MWENYEKITI NA MKURUGENZI 2

MAFANIKIO MAKUU TACRI 2003 - 2004 4

IDARA YA UBORESHAJI WA ZAO 5

Uchunguzi Kifani:

*Mustakabali wa kahawa Tanzania baada ya kuidhinishwa kwa aina mpya chotara zinazostahimili magonjwa* 6

Uchunguzi Kifani:

*Ugonjwa wa mnyauko fuzari: tishio kwa ustawi wa wakulima wa kahawa ya Robusta Kagera.* 7

IDARA YA TIJA NA USINDIKAJI WA MWANZO WA ZAO 8

Uchunguzi Kifani

*Kilimo mseto cha kahawa na migomba: Faida za Kiuchumi* 10

IDARA YA VIRUBITISHI VYA ZAO 11

Uchunguzi Kifani

*Utumiaji Halisi wa Mbolea kwenye Kilimo cha Msongamano* 12

IDARA YA USAMBAZAJI TEKNOLOJIA NA MAFUNZO 13

Uchunguzi Kifani

*Uzalishaji kwa wingi miche ya vikonyo: Changamoto ya Uzalishaji Kahawa kwa Faida* 15


Uchunguzi Kifani

*Mfano wa mafanikio ya ushirikiano wa maadili na kupeana moyo* 16

IDARA YA UHAKIKA WA RIZIKI NA MAPATO 17

RAMANI YA MAENEO YANAYOLIMA KAHAWA TANZANIA 18

# UJUMBE WA MWENYEKITI NA MKURUGENZI



## TAARIFA YA MWENYEKITI

Inanipa faraja kubwa kuandika kwa mara nyingine dibaji hii kwa Taarifa ya Mwaka wa pili kwa Taasisi ya Utafiti wa Kahawa. Hii ni hatua nyingine muhimu kwa hii Taasisi yetu changa.

Katika dibaji yangu kwenye Taarifa ya Mwaka wa kwanza, niliandika kwamba TaCRI imeanza vizuri na kwamba wadau walikuwa na matarajio makubwa kutoka kwa Taasisi yetu. Ninayo furaha kusema kwamba utendaji umevuka matarajio katika kipindi hiki cha mwaka. Vipaumbele vyetu vya juu vilikuwa ni kubainisha teknolojia bora za kahawa zilizopo kutokana na utafiti uliofanyika nchini miaka ya nyuma kwa kipindi cha takribani nusu karne, na kuweka mkazo wa haraka katika kutoa na kusambaza aina mpya bora za kahawa zenye mwonjo mzuri na zisizoshambuliwa na magonjwa kama walivyoelekeza wadau. Aina hizi mpya bora ndio tegemeo pekee kwa wakulima wa kahawa Tanzania, katika hali halisi ya sasa ya gharama kubwa za uzalishaji na bei duni sana za kahawa kuliko wakati wowote ule. Ninafurahi kuona kwamba kumekuwa na maendeleo makubwa katika vipaumbele hivi kama inavyoelezwa katika Taarifa hii.

Kwa niaba ya wazalishaji wote wa kahawa Tanzania, ninapenda kutoa shukrani zetu kwa serikali kwa juhudi zake za kutia moyo kuhakikisha kwamba hatua sahihi zinatekelezwa ili kuiweka tasnia ya kahawa kwenye mkondo wa maendeleo. Hatua hizi, ikiwa ni pamoja na utoaji wa awali wa aina hizi mpya bora za kahawa ya Arabika, hazingewezekana bila msaada mkubwa wa Muungano wa nchi za Ulaya (EU), ambao tunashukuru sana.

Ni mategemeo yangu kwamba Serikali na Muungano wa nchi za Ulaya, wataendelea kutoa msaada huu kwa TaCRI na kwa tasnia ya kahawa kwa ujumla, kuongezea kwenye mchango wa wazalishaji, ili zao la kahawa liweze kurudia tena nafasi yake kama nguzo muhimu katika uchumi wa taifa.

Ninasikitika kwamba nafasi muhimu za wataalamu wa TaCRI hazikujazwa katika kipindi hiki kwa sababu mbali mbali. Tunatarajia kwamba hatua madhubuti zitachukuliwa katika kipindi kijacho ili kusahihisha pengo hili ili tupate wataalamu wenye uwezo na ari ya kutosha kukamilisha timu ya TaCRI.

Kwa niaba ya wadau wote wa kahawa na Bodi ya Wakurugenzi ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa menejimenti na wafanyakazi wa TaCRI kwa bidii zao na mafanikio mazuri katika kipindi cha mwaka uliopita na kutekeleza wajibu wao kwa wadau.

Edwin I. M. Mtei
Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi



## TAARIFA YA MKURUGENZI MKUU MTENDAJI

Tumekuwa na maendeleo muhimu TaCRI. Tumekamilisha mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mkakati wa Miaka Mitano na kujiandaa kwa mwaka wa pili wa utekelezaji.

Fanikio letu muhimu kabisa kipindi hiki ni utoaji wa awali wa aina zetu mpya bora za kahawa chotara zinazozaa kwa wingi na zenye mwonjo mzuri. Hii ni hatua madhubuti na muhimu ya kuanzia ili kuharakisha uzalishaji na usambazaji wa aina bora za kahawa kwa wazalishaji nchi nzima.

Tulifikia lengo letu la kuwa na bustani mama ya msingi Lyamungu yenye miti mama 10,000 ya hizi aina bora chotara. Tulipanua na kuboresha ujuzi wa kuzalisha miche

ya vikonyo kufikia mafanikio ya zaidi ya 90%. Tumeboresha pia ujuzi wa upachikizaji kufikia mafanikio ya 100%.

Vituo vyetu vidogo vya utafiti vya kanda Tanzania nzima vimekamilika na kuanza kazi baada ya kuajiri wataalamu watakaoshughulikia uboreshaji wa uzalishaji kahawa katika kanda zote.

Katika ushirikiano wa kimataifa, tumekamilisha mazungumzo na kituo cha utafiti cha Ufaransa (CIRAD) ili kuanza kujenga maabara ya kuzalisha miche ya kahawa Lyamungu kwa njia ya chupa yenye uwezo wa kuzaisha miche 100,000 — 150,000 kwa mwaka. Tulipiga hatua pia katika kuanzisha ushirikiano na kituo cha utafiti wa magonjwa ya kahawa cha Ureno, CIFC, ili kuimarisha utafiti wa kutoa aina bora za kahawa zisizoshambuliwa na magonjwa ya chulebuni na kutu ya majani.

Tulifaidika pia na msaada wa Programu ya Uholanzi ya kutoa ushauri wa menejimenti (NMCP) ambayo ilifadhili mtaalamu bingwa wa utafiti wa kahawa kutembelea TaCRI kwa ushauri Januari mwaka huu. NMCP itaendelea kufadhili wataalamu wengine kutembelea TaCRI kwa ushauri kila itakapohitajika. Pia tulianza mazungumzo ya awali na Chuo Kikuu cha Sweden cha Sayansi ya Kilimo, Alnarp ili kuanza ushirikiano katika utoaji wa aina bora za kahawa na kuzizalisha kwa chupa. Tuliimarisha pia ushirikiano wa kikanda kwa kushiriki kwenye mkutano wa uzinduzi wa mtandao wa utafiti wa kahawa Afrika ya Mashariki (CORNET) na kwenye mtandao wa utafiti wa kahawa Afrika (ACRN). Na mwisho, tulifadhili wafanyakazi kushiriki kwenye kongamano muhimu zinazohusu kahawa ikiwa ni pamoja na kushiriki kwenye mkutano na maonyesho ya kwanza ya chama cha ushirikiano wa kuzalisha kahawa bora cha Afrika ya Mashariki (EAFCA), Nairobi Februari 2004 na wa chama cha kahawa bora cha Marekani (SCAA), Atlanta mwezi April 2004.

Tulipanua programu yetu ya mafunzo ya wakufunzi wa ugani ili kutoa mafunzo kwa vikundi vya wakulima. Tuliimarisha pia mafunzo ya wakulima kwa vikundi kwenye wilaya ya Mbinga ambayo tayari yameleta mafanikio ya uzalishaji kahawa bora Mbinga na kuinua kipato cha wazalishaji.

Katika kipindi hiki tuliweka mkazo mkubwa wa kuitangaza TaCRI na huduma zake kwa wadau. Kwa mfano, mwanzo wa Juni tulikuwa na sikukuu ndogo ya wakulima wakubwa (Estates) na wanunuzi wa kahawa (TCA) kujadiliana juu ya umuhimu mkubwa wa aina mpya chotara za kahawa. Tulitembelewa pia na kamati ya Bunge ya Ardhi na Kilimo Januari mwaka huu na pia Kamishna wa Muungano wa nchi za Ulaya wa Maendeleo na Misaada ya Kibinadamu mwishoni mwa mwaka jana. Sikukuu za wakullima za mafanikio makubwa zilifanyika Lyamungu na Ugano kipindi hiki. Tumeanza pia mpango wa kutoa vipeperushi vyenye maelezo rahisi ya taarifa za ugani kwa ajili ya kuvisambaza kwa wakulima. Usambazaji wa taarifa za TaCRI utapanuka zaidi mwaka ujao wakati mkakati wetu wa mawasiliano utakapoanza kutekelezwa.

Kazi mpya zilizoanzishwa ni pamoja na kuanza utekelezaji wa mkakati wa kudhibiti mnyauko fuzari wa kahawa ya Robusta mkoa wa Kagera na kuanza mkakati wa kutoa aina bora za kahawa chotara fupi. Pia tuna nembo mpya.

Uwezo wetu wa kutoa huduma kwa manufaa ya wadau wote inategemea watumishi. Ninafurahi kusema kwamba tuna timu ya watumishi bora TaCRI. Tulikuwa na warsha ya kujenga timu Agosti 2002 iliyofuatiwa na warsha ya menejimenti ya utendaji Novemba 2003. Tuko kwenye hatua za mwanzo za utekelezaji wa mfumo wa menejimenti ya utendaji kuhakikisha kwamba tunapata utendaji bora kabisa kutoka watumishi wetu na wakati huo huo tunawasaidia watumishi wafikie uwezo wao.

Kwa kifupi, huu ni muhtasari wa mafanikio yetu kwa mwaka uliopita. Mtasoma ushahidi wa mafanikio yetu na shughuli zilizopendekezwa kwa mwaka ujao kwenye Taarifa hii.

Ninawatakieni mwaka mpya wenye mafanikio na ninapenda kuwakaribisha sana wadau wetu wote kututembelea Lyamungu na vituo vyetu vidogo Maruku, Mbimba na Ugano. Tunao usemi mzuri kwamba kila siku TaCRI ni sikukuu ya walikuma! Karibuni sana.

Profesa James M. Teri
Mkurugenzi Mkuu Mtendaji.

# MAFANIKIO MAKUU TACRI 2003 - 2004

Taarifa kamili za mafanikio ya mwaka uliopita na vipaumbele vya miezi 12 ijayo vinaelezwa katika kurasa zifuatazo kwa kila idara ya TaCRI. Vipengele muhimu vinatolewa kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

### Utoaji wa Awali wa Aina 5 za Mibuni Iliyoboreshwa

Mwezi Machi Taasisi ilifikia hatua muhimu wakati Kamati ya Taifa ya Aina na Udhibiti wa Mbegu ilipoidhinisha utoaji wa awali wa aina tano mpya bora za kahawa chotara. Kila moja ya aina hizo mpya inastahimili ugonjwa wa chulebuni na kutu ya majani, inazaa kwa wingi na ina ubora wa hali ya juu. Manufaa ya aina hizi mpya ni kubwa kwa kuwa zitapunguza gharama za uzalishaji kwa hadi 50%, huku wakulima kutolazimika tena kunyunyizia dawa dhidi ya magonjwa.

### Vikundi vya Wakulima Vyaanza Uzalishaji Miche ya Aina Mpya Bora

Idara ya Tija na Usindikaji wa Mwanzo wa Zao ikishirikiana na Idara ya Usambazaji Teknolojia na Mafunzo imetoa zaidi ya miche 70,000 ya vikonyo ya aina tano mpya zilizoidhinishwa. Kati ya hizi, 18,000 zimekwishasambazwa kwa vikundi vya wakulima ambavyo navyo vimefunzwa namna ya kuanzisha bustani zao za bei nafuu za kuzalisha na kuisambaza kwa mkulima mmoja mmoja.


### Mwongozo wa Mafunzo Watolewa

Idara ya Usambazaji Teknolojia na Mafunzo imetoa mwongozo wa mafunzo na kielelezo cha uzalishaji kwa vikonyo. Mwongozo huu unatumiwa na maafisa ugani na wasimamizi wa bustani ili kuhimiza uzalishaji na usambazaji wa hizi aina mpya. Mpaka sasa, vikundi 27 vya wakulima na bustani kuu mbili zimenufaika na mafunzo haya.

### Mimea Iliyozalishwa kwa Chupa Yastawi Vizuri.

Aina 9 zilizozalishwa kwa chupa zilipandikizwa mwaka 2002 kwenye maeneo tofauti yanayolima kahawa nchini. Maendeleo yake ni mazuri sana katika kuzaa kwa wingi na kustahimili magonjwa ya chulebuni na kutu ya majani.


# MUUNDO WA TaCRI



# IDARA YA UBORESHAJI WA ZAO

**Tija duni ya kahawa nchini inachangiwa na kuendelea kulima aina zinazoathiriwa na magonjwa. Majukumu ya Idara ya Uboreshaji wa Zao ni kuhakikisha kwamba aina bora za Arabika na Robusta zinazozaa kwa wingi, zinazostahimili magonjwa, zenye ubora wa hali ya juu zinapatikana na kusamabazwa kwa wakulima. Tayari mafanikio yamepatikana kwenye kahawa aina ya Arabika ambapo aina mpya bora zimeanza kusambazwa kwa wakulima.**

## MAFANIKIO MAKUU 2003-2004



*Aina mpya zilizooteshwa Lyamungu*

- Mwezi Machi Kamati ya Taifa ya Aina na Udhibiti wa Mbegu, iliidhinisha rasmi utoaji awali kwa wakulima aina 5 bora za kahawa ya Arabika. Aina hizi 5 zina tija ya juu, hustahimili magonjwa ya chulebuni na kutu ya majani, na zina ubora wa juu unaokubalika kimataifa.
- Kukamilisha ufafanuzi wa kina wa aina hizi 5 kulingana na vifafanuzi vya kimataifa.
- Kukamilisha vichavulio 67 kwa kutumia aina 32 za mibuni mbilikimo kutoka Colombia, na mibuni 61 mirefu kutoka shamba namba 23. Kati ya hizo, kahawa vichavulio 20 vilichaguliwa kuwa bora zaidi.
- Aina 9 za kahawa chotara zilizozalishwa kwa njia ya chupa (Tissue Culture) na kuoteshwa katika mashamba darasa mtawanyiko 25 kati ya mwishoni mwa 2001 na katikati ya 2002, zinaendelea kuonyesha ustawi mzuri na ustahimilivu wa magonjwa ya chulebuni na kutu ya majani.
- Vikonyo toka aina bora 20 vilivyochaguliwa toka shamba namba 23 vimeandaliwa kwa lengo la kuanzisha majaribio mtawanyiko awamu ya pili mwaka 2005.
- Mpango wa kuchagua aina za kahawa ya Robusta zenye kustahimili ugonjwa wa mnyauko fuzari umeanza ambapo aina 67 za Robusta zimeambukizwa viini vya ugonjwa wa mnyauko fuzari. Kufikia mwaka 2005 inatarajiwa aina 216 za Robusta zitakuwa zimefanyiwa utafiti.
- Jumla ya mibuni 15 ya Robusta inayoelekea kustahimili ugonjwa wa mnyauko fuzari ilibainika katika maeneo makuu yanayokabiliwa na ugonjwa huu.
- Mpango wa kudhibiti mnyauko fuzari ulitekelezwa kwa kutokomeza baadhi ya mibuni iliyoathirika. Katika kipindi cha mwaka huu, 20% ya mibuni iliyoathirika iling'olewa katika wilaya za Bukoba, Muleba na Karagwe. Ili kueneza uelewa na kupunguza ueneaji wa ugonjwa huu, wakulima 1382 na maafisa 98 wa ugani walifunzwa udhibiti wa ugonjwa huu.

## VIPAUMBELE VIKUU 2004-2005


- Kwa kushirikiana na wakala wa kuidhinisha aina bora na uthibitisho wa mbegu (TOSCA), TaCRI inadhamiria kukamilisha uainishaji wa takwimu za uimara wa aina 5 za mibuni zilizoidhinishwa, ili kukidhi vigezo vitakavyowezesha kupitishwa rasmi.
- Kushirikiana na ARI Mikocheni ili kupata ramani ya chembe nasaba za kahawa chotara zilizopo kwa minajili ya kupata haki miliki (patent).
- Kuendelea kutafiti aina mbilikimo chotara za kahawa zenye tija ya juu, zinazostahimili magonjwa na zenye mwonjo mzuri.
- Kukamilisha mpango wa kuwa na maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa (Tissue Culture) kwa lengo la utafiti TaCRI, Lyamungu ifikapo mwishoni mwa 2005. Mpango huu unashirikisha taasisi ya utafiti ya Ufaransa (CIRAD).
- Kuendeleza utafiti wa Robusta kutambua aina zinazostahimili athari za ugonjwa wa mnyauko fuzari.
- Kuanzisha mpango kabambe wa uonjaji kahawa bora kwa kutumia taasisi za nchi za kanda ya mashariki na za kimataifa.

# UCHUNGUZI KIFANI

## *Mustakabali wa kahawa Tanzania baada ya kuidhinishwa kwa aina mpya chotara zinazostahimili magonjwa*

Idhini rasmi ya awali iliyotolewa Machi 4, 2004 na Kamati ya Taifa ya Aina na Udhibiti wa Mbegu kwa aina 5 za kahawa zilizoboreshwa, imefungua sura mpya kwa tasnia ya kahawa nchini Tanzania. Hatimaye sasa wakulima wa kahawa Tanzania watafaidika na kuwa na aina ya kahawa iliyoboreshwa.

- Tija ya juu: Mavuno yanaanzia kilo 1,961 — 2,763 kwa hekta kwa N 39 (34.6 — 115% zaidi ya N 39) bila gharama za kunyunyizia madawa pia.
- Punje kubwa: Zaidi ya asilimia 59% ya punje hufikia ukubwa wa AA ikilinganishwa na 37% ya aina za sasa (N 39) na 78% AA+A ikilinganishwa na 53% kwa N 39.
- Muonjo mzuri: Muonjo ni sawa au zaidi ya N 39 (daraja la 4 — 6), muonjo mzuri, wa uhakika na harufu nzuri.
- Kustahimili chulebuni na kutu ya majani: Umuhimu wa hizi aina mpya bora utakuwa mkubwa kwa kupunguza gharama za uzalishaji kwa 50% kwa sababu hakutakuwa na haja ya kunyunyizia madawa. Tasnia ya kahawa imekuwa ikitumia dola za kimarekani milioni 40 kila mwaka kwa madawa ya kudhibiti chulebuni na kutu ya majani.
- Maotea machache: Hii inapunguza gharama za kukatia matawi ambayo inapunguza gharama za uzalishaji pia. Mti uliowazi unapunguza ushambulizi pia wadudu waharibifu.
- Inasisitizwa kwamba aina hizi bora hazina mbegu kutoka aina za Catimor na kwamba hazijazalishwa kwa kutumia viumbe (GMOs).




*Wakulima wadogo na wenye mashamba makubwa wanahimizwa kutumia aina hizi mpya kutokana na manufaa yake ikilinganishwa na aina za kibiashara zilizopo sasa.*




*Wadau wakitafakari ubora wa aina mpya za kahawa kulinganisha na aina za sasa.*

# UCHUNGUZI KIFANI

*Ugonjwa wa mnyauko fuzari: tishio kwa ustawi wa wakulima wa kahawa ya Robusta Kagera.*



*Mbuni aina ya Robusta ulioathirika na mnyauko fuzari*

Kahawa aina Robusta ni zao muhimu kwa wakulima wa mkoa wa Kagera, linategemeza kaya takribani 70,000. Hivi karibuni zao hili limeathiriwa sana na ugonjwa wa mnyauko fuzari; ugonjwa unaoshambulia mifumo inayopitisha maji na virutubisho toka ardhini, kwa haraka hutokeza mnyauko na kukauka kwa mti wa kahawa.

Kwa wastani uzalishaji wa kahawa aina ya Robusta hupatia wadau dola za kimarekani milioni 11 hivi kwa mwaka. Tokea mlipuko wa ugonjwa huu mwaka 1997, takribani tani 300 zimeripotiwa kupotea kwa mwaka zenye thamani ya dola za kimarekani 200,000.

Kwa kushirikiana na wadau wa ndani ya nchi na taasisi za kimataifa za kisayansi kama vile CABI ya Uingereza na CIRAD; TaCRI imeanzisha mipango mbalimbali kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huu hatari:

- Mzunguko ulifanywa nchi nzima kunakostawisha kahawa kufahamu mweneo na kiwango cha ugonjwa. Mnyauko fuzari umeonekana kuathiri kahawa aina ya Robusta pekee.
- Jumla ya wakulima 1382 na maafisa ugani 98 walioko Kagera wamefundishwa mbinu za kudhibiti kuenea ugonjwa huu. Mafunzo yanahusu kutambua dalili za ugonjwa, na kuharibu mibuni iliyoathirika kuzuia usambaaji zaidi.
- Mpango wa kung'oa ulianza Bukoba, Muleba na Karagwe. Kati ya mibuni 5000 iliyokadiriwa kuathiriwa na ugonjwa wa mnyauko fuzari mapema 2003, mibuni 1402 imeshang'olewa na kiasi kikubwa kupunguza vyanzo vya usambaaji.
- Ili kuongeza ufahamu wa ugonjwa huu makala ziliandikwa kwenye magazeti, taarifa katika vipindi vya radio na runinga na uandaaji wa vitini ili kuwapa taarifa wakulima juu ya hatari na athari za ugonjwa huu.
- Vikao vya viongozi wa kiserikali vimetumika katika kueneza taarifa za ugonjwa wa mnyauko fuzari. Kwa mfano mwezi Mei mwaka uliopita, TaCRI na wawakilishi wa Wizara ya Kilimo na Chakula walialikwa kuhudhuria kamati kuu inayoratibu shughuli za maendeleo mkoa Kagera chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa Kagera Meja Jenerali Tumainieli Kiwelu. Mikakati ya kudhibiti ugonjwa wa mnyauko fuzari iliwasilishwa. Kikao kiliunga mkono ung'oaji mibuni iliyoathirika na mafunzo kwa maafisa ugani na wakulima kutumia fedha toka halmashauri za wilaya.
- Majaribio ya muda mfupi yanayohusisha matumizi ya viua ukungu na utunzaji yalianzishwa mwaka 2003 sehemu 12 katika wilaya za Bukoba na Karagwe. Huu ni mwaka wa pili na maendeleo yanaridhisha.
- Uchambuzi wa aina zinazostahimili ugonjwa huu unaendelea. Kati ya aina 216 zilizopo Maruku, aina 67 zimefanyiwa uambukizaji viini vya ugonjwa na dalili zimeanza kujitokeza. Kuna aina zinazoonyesha kuathiriwa mapema. Jitihada za kuongeza aina zinazostahimili zinaendelea kufanyika. Mpaka sasa mibuni 15 inaonyesha uwezo wa kustahimili katika maeneo yaliyoathirika sana

# IDARA YA TIJA NA USINDIKAJI WA MWANZO WA ZAO


Idara ya Tija na Usindikaji wa Mwanzo wa Zao inaongoza katika kuendeleza mbinu bora za utunzaji na udhibiti husishi wa visumbufu vya zao vinavyofaa kutumika katika mifumo mbalimbali ya ulimaji wa kahawa nchini. Lengo ni kuongeza uzalishaji kwa eneo au kwa mti, kupunguza gharama za uzalishaji, na kuongeza kiwango cha ubora wa usindikaji wa mwanzo.



*Mkulima akifundishwa kupandikiza aina ya kahawa iliyoboreshwa kwenye mti wa kahawa wa zamani*

## MAFANIKIO MAKUU: 2003—2004

- Mpaka sasa zaidi ya miche 70,000 inayozalishwa kwa njia ya vikonyo ipo katika hatua mbalimbali za kuandaliwa kwenye vitalau, tayari kusambazwa kwa wakulima ambao nao wataanzisha vitalu vyao wenyewe vya kustawisha miche zaidi kwa kushirikiana na Idara ya Usambazaji Teknolojia na Mafunzo. Usambazaji unaelendelea.
- Teknolojia 8 za utunzaji mimea na udhibiti husishi wa visumbufu vya zao zimeandaliwa na zitasambazwa kwa wakulima kwa njia ya vijarida na mabango. Haya yatakuwa na maelezo kuhusu uchanganyaji wa mazao, upogoaji, usindikaji na visumbufu vikuu vya mibuni (kidomozi, kimatira, ruhuka, bungua mweupe, na vidung'ata). Kwa sasa vielelezo hivi vimekamilika tayari kwa kujaribiwa na wakulima kwa ushirikiano na Idara ya Usambazaji Teknolojia na Mafunzo.
- Maelezo kuhusu utunzaji wa mibuni yamechapishwa na yamekuwa kama mwongozo utakaotumika kuandaa mifano kwenye mashamba katika kanda mbalimbali za kiekolojia za ulimaji wa kahawa.
- Kukamilika kwa mbinu ya upachikizaji wa machipukizi ya miche bora ya mibuni chotara kwenye mashina ya mibuni aina ya zamani ikiwa kama njia mbadala ya ukarabati wa mashamba chakavu. Mafanikio kati ya 70 - 90% yamepatikana. Zaidi ya miti 1,000 imekwishapatachikizwa Lyamungu.
- Virutubisho mbali mbali vitumikazo kwenye makasha ya kuzalishia vikonyo tofauti na mchanga asilia wa Kisangiro na udongo wa msituni umefanyiwa utafiti. Hii ni faida kubwa kwa wakulima pale ambapo aina hizi za mchanga au udongo wa msituni havipatikana kwa urahisi.
- Zaidi ya sampuli 100 kwa ajili ya tathmini ya muonjo zilipelekwa kwenye asasi mbalimbali za Tanzania na nje. Sampuli hizo zilikuwa pamoja na aina 5 mpya zilizopata idhini ya kutolewa, 77 toka aina bora na 33 toka shamba la 23 ambalo limetengwa kwa ajili ya kupata aina nyingine fupi bora. Matokeo ni mazuri sana.
- Nakala ya kwanza ya taarifa kuhusu udhibiti husishi wa visumbufu vya mibuni (IPM) imetayarishwa na maandalizi ya majaribio ya IPM yameshaanza.
- Uchunguzi wa kutafuta wadudu rafiki wa visumbufu vya mibuni kama vile kimatira, kidomozi na vidung'ata ulianza kituoni na vijiji vya jirani.
- Mtumishi mmoja alihudhuria mafunzo ya mwezi mmoja kuhusu hali ya hewa ambayo yaliendeshwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa.
- Mtafiti wa kimataifa kuhusu kahawa, Dr. Herbert van der Vossen, alirejea kutoa msaada wa kitaalamu idarani January 2004.



*Bustani mpya ya mimea inayodhibiti wadudu waharibifu*

# IDARA YA TIJA NA USINDIKAJI WA MWANZO WA ZAO

VIPAUMBELE VIKUU: 2004—2005

- Kuajiri bingwa wa IPM.
- Kuanzisha majaribio ya utunzaji wa aina mpya za mibuni pamoja na kuainisha kiasi kidogo cha virutubishi vya shaba kwenye morututu kwenye aina mpya.
- Kukarabati na kuweka vifaa sehemu ya kufugia wadudu.
- Kukarabati na kuweka vifaa kwenye maabara ya Udhibiti Husishi wa Visumbufu vya Zao.



*Udhibiti asili wa wadudu waharibifu*


- Kukarabati kiwanda kidogo cha usindikaji cha Lyamungu ambacho kinatumika kusindika sampuli za kahawa kwa ajili ya uonjaji na kuendesha mafunzo ya watumishi ya mbinu za uandaaji wa sampuli kwa muonjo.
- Kushirikiana na Idara ya Uboreshaji wa Zao ili kutekeleza vipengele vya kipekee (DUS) kwa aina za kahawa zilizopata idhini ya awali.
- Kushirikiana na Idara ya Usambazaji Teknolojia na Mafunzo kuanzisha majaribio na maonyesho ya mashambani ya teknolojia mpya, ikiwa ni pamoja na upogoaji, maandamo ya ubadilishaji, matumizi ya mboji, matandazo na upachikizaji ili kuboresha tija na ubora wa kahawa.
- Kushiriki katika uzalishaji wa miche ya vikonyo vya aina chotara kwa ajili ya utafiti na usambazaji na Idara ya Usambazaji Teknolojia na Mafunzo.
- Kushirikiana na Idara ya Usambazaji Teknolojia na Mafunzo kuandaa ujumbe wa ugani kuhusu ukaushaji kwenye kivuli dhidi ya jua, na jua dhidi ya ukaushaji kwa kutumia njia bandia, kwa kuzingatia ubora wa kahawa.
- Kukusanya na kutawanya habari za hali ya hewa kutoka Lyamungu na vituo vingine vya TaCRI.

# UCHUNGUZI KIFANI

## *Kilimo mseto cha kahawa na migomba: Faida za Kiuchumi*

Kilimo mseto cha kahawa na migomba ni mfumo unaotumika zaidi na wakulima wadogo Tanzania katika maeneo ya Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, na Kagera. Kilimo hiki mseto kina manufaa makubwa kwa mkulima mdogo kuliko kahawa pekee.

Ukubwa wa mashamba mseto ya kahawa na migomba ni kama eka 3 kwa wastani, migomba ikiwa ndio zao kuu la chakula na kahawa zao la biashara. Kipindi hiki cha bei duni ya kahawa kimewafanya wakulima wengi kulipuuza zao la kahawa na kushikilia zaidi ndizi, na hivyo kupunguza sana kipato cha shamba. Gharama za juu za uzalishaji, hasa katika kudhibiti magonjwa ya chulebuni na kutu ya majani pia kumechangia kushusha vipato vya wakulima hasa kwa zao la kahawa.



*Mchanganyiko holela wa kahawa na migomba usioleta tija*

Hatua ya kwanza ambayo imechukuliwa na TaCRI katika kulikabili tatizo hili ni kutoa kahawa chotara iliyoboreshwa na ambayo inastahimili magonjwa ya chulebuni na kutu ya majani.

Katika mtazamo mahususi wa hiki kilimo mseto, majaribio na utafiti ulifanyika mashambani kutumia hizi aina bora za kahawa, kwanza kuzitathmini kwenye kumudu mfumo wa mseto na migomba, halafu pili kubaini jumla ya kahawa/migomba ambayo itakuwa na faida kubwa zaidi kiuchumi kwa eneo.

Utafiti umebaini mpangilio sahihi wa shina moja la mgomba kwa mibuni 6, ikilinganishwa na mtindo wa asili ambao wakulima hupendelea kuweka shina moja la mgomba kwa mbuni mmoja.

Matokeo haya ni dhahiri kabisa kiuchumi. Jumla ya mapato yaliyotokana na mfumo huu mpya yalikuwa 50% zaidi ya kuwa na shamba la kahawa pekee, na 42% zaidi ya kuwa na shina moja la mgomba kwa mbuni mmoja.

Matokeo ya utafiti huo yamechapishwa katika vijarida na miongozo kwa ajili ya wakulima. Kwa muhutasari, ili kutumia vyema ardhi ndogo iliyopo, TaCRI inapendekeza kwa wakulima wadogo wadogo kwenye maeneo yanayostahili, kufuata mtindo ufuatao wa kuchanganya mazao:-

- **Pandikiza mstari mmoja wa migomba kila baada ya mistari mitatu ya kahawa.**
- **Pandikiza kwa nafasi kwa kufuata vipimo vifuatavyo: acha nafasi ya mita 2.5 kati ya kila mstari wa kahawa na mita 1.25 kati ya mmea na mmea ndani ya mstari.**
- **Kwa hali hiyo, mistari ya migomba itaachana kwa mita 10. Acha nafasi ya mita 2.5 kati ya shina moja la mgomba na lingine.**
- **Tumia debe moja au mawili ya samadi wakati wa kupanda.**

Utafiti huo unabainisha wazi kwamba kwa kutumia mtindo huu, uzalishaji na mapato ya mkulima yote yanaongezeka.

Uendelezaji wa mbinu za ukulima wa zao na teknolojia bora za utunzaji wa mimea ni sehemu muhimu ya shughuli za TaCRI na utafiti unaendelea kubaini teknolojia nyingine nafuu na rahisi kutekeleza na wakati huo huo zinaongeza kipato.

# IDARA YA VIRUBITISHI VYA ZAO

Idara ya Virutubishi vya Zao imelenga katika kuendeleza na kusambaza mifumo ya usimamizi wa gharama nafuu za urutubishaji ili kuwawezesha wakulima kufanya maamuzi mwanana kuhusu njia bora kwao kudhibiti rutuba katika ardhi yao. Idara pia inahusika katika kutoa tathmini za udongo na mimea na kutoa taarifa za michakato, na kuwaunganisha wakulima na maabara nyingine zinazofanya tathmini ya udongo na mimea nchini.



*Uchambuzi wa udongo kwenye maabara*

## MAFANIKIO MAKUU 2003 - 2004

- Uainishaji wa teknolojia zilizopo ulikamilika iliyosaidia kutoa vipeperushi vya mbolea ya chumvi chumvi, samadi na mbolea ya Minjingu. Hivi vipeperushi vitatathminiwa kwa wakulima na Idara ya Usambazaji Teknolojia na Mafunzo.
- Maandalizi yalikamilika kwa kushirikiana na idara nyingine kuanzisha majaribio ya mashambani ya usimamizi wa kudhibiti rutuba katika ardhi (ISFM).
- Idara iliendelea kutoa ushauri kwa wakulima kutoka wilaya za Hai na Moshi Vijijini kuhusu masuala yanayohusiana na virutubishi ardhini na matatizo ya virutubishi kwenye kahawa.
- Jumla ya sampuli 89 za udongo kutoka katika maeneo ya majaribio zilikusanywa na kufanyiwa tathmini kubaini vigezo halisi vya urutubishaji wa udongo.
- Huduma za ushauri zilitolewa kwa idara za utafiti kuhusu vipimo vya kurekebisha mapungufu ya virubitishi kwenye udongo.

## VIPAUMBELE VIKUU 2004 — 2005

- Kuandaa ziara za ushauri kutoka kwa wataalamu wa kimataifa.
- Kukarabati maabara ya virutubishi vya zao, ikiwa ni pamoja na ununuzi na uwekaji wa vifaa.
- Kuendelea kusimamia majaribio kwenye vituo.
- Kushirikiana na Idara ya Usambazaji Teknolojia katika kuonesha mifanano na majaribio mashamabani ya ISFM.
- Kubaini kiwango kinachofaa zaidi cha mchanganyiko wa samadi na mbolea ya kemikali ili kuwa na uzalishaji endelevu wa kahawa ya Arabika.
- Kufanya utafiti wa uhifadhi na urutubishaji wa ardhi kwa kutumia marejea, miti kivuli, mboji, vyanzo vya lishe na kuzuia mimomonyoko ya ardhi.
- Kubaini viwango vya mbolea vinavyohitajika kwa aina za chotara za Arabika ambazo zinastahimili magonjwa na zenye tija ya juu.
- Kulinganisha kipato kiuchumi kutokana na kahawa iliyokuzwa bila kemikali (strictly organic) na zile zilizokuzwa kwa kutumia pembejeo za kawaida za kahawa.
- Kulinganisha ubora wa udongo na hali ya virutubisho kwenye mashamba yasiyotumia kemikali na yale yanayotumia pembejeo za kawaida.
- Kuhakiki hali ya virutubisho kwenye majaribio yote ya mashambani ya idara zote za TaCRI.
- Kufuatilia kupungua kwa hali ya virutubisho kwenye mashamba ya kahawa ya wakulima wadogo.
- Kufanya kazi kwa karibu na wadau na kufanya mapitio ya mara kwa mara ya maendeleo.



*Wataalam wakichukua sampuli za udongo kwa ajili ya uchambuzi.*

# UCHUNGUZI KIFANI

## *Utumiaji Halisi wa Mbolea kwenye Kilimo cha Msongamano*

Katika kipindi cha mwaka uliopita, Idara ya Virutubishi vya Zao imekuwa ikitafiti matumizi halisi ya mbolea kulingana na ongezeko la msongamano wa kahawa kwa eneo kwenye mashamba makubwa (estates). Matokeo yalionesha kuna ongezeko kubwa la mavuno ya kahawa kwa kuongeza msongamano wa miti ya kahawa (ya aina ya zamani ndefu) kutoka mibuni 1330 kwa hekta na kufikia kati ya mibuni 3,200 hadi 5,000 kwa hekta. Utafiti umebaini kwamba mibuni ikizidi 5,000 kwa hecta, matawi ya mibuni yanazuia shughuli za shambani na wakati huo kunakuwepo ongezeko la dhahiri la mimea kugombea mwanga, lishe na maji.

Kwa upande wa lishe ya mibuni, ili kufaidika kimavuno kutokana na kusonganisha mimea, ni budi kuongeza utumiaji wa mbolea ya N kuweka kiasi cha kilo 60 za N kwa hekta mara tatu. Hii inatoa nafasi ya kusonganisha mibuni na wakati huo huo kuongeza mavuno au kutoa nafasi ya kuweka eneo la ardhi kwa matumizi mengine kwenye maeneo yanayolima kahawa yenye ufinyu wa ardhi.

# IDARA YA USAMBAZAJI TEKNOLOJIA NA MAFUNZO


Wakulima wakipata mafunzo ya kilimo bora

Idara ya Usambazaji Teknolojia na Mafunzo ina nafasi muhimu ya kuwa kioo cha shughuli zote za TaCRI. Idara ina wajibu wa kusambaza matokeo
ya utafiti wa TaCRI kwa tasnia ya kahawa na hususan kutoa na kusambaza teknolojia zinazofaa kwa wakulima na asasi shiriki.

Majukumu mengine makuu ya Idara ni pamoja na kuzalisha na kusambaza kwa wingi aina mpya bora za kahawa kwa wakulima nchi nzima.

Watumishi bora waliajiriwa mwaka 2004 kusaidia kutekeleza malengo yetu makubwa tuliyojiwekea. Kwa sasa Idara iko kwenye hatua za kuandaa mkakati wa mawasiliano utakaokamilika mwishoni mwa 2004.

## MAFANIKIO MAKUU 2003 - 2004

- Sehemu mpya ya kukuzia vikonyo (VPU) ilijengwa, ambayo inaongeza kiwango cha kuzalisha kwa wingi aina mpya chotara kufikia vikonyo 136,000.
- Uhariri wa vipeperushi na mabango vya teknolojia zilizobainishwa ulikamilika. Mpaka sasa, vipeperushi 13 na mabango mawili yamekamilika.
- Mafunzo kwa vikundi 15 vya wakulima vijijini yalifanyika katika wilaya ya Mbinga. Vikundi vingine 13 vya wakulima vilisaidiwa na TaCRI kuuza kahawa yao moja kwa moja mnadani, na matokeo yake ni kwamba vikundi hivyo viliweza kupata wastani wa bei ya shilingi 751 kwa kilo, ikilinganishwa na bei ya shambani ya shilingi 350 kwa kilo.
- Tulitoa mwongozo wa mafunzo ya uzalishaji wa miche kwa vikonyo. Mwongozo huu umeanza kutumika kwa mafunzo ya watumishi wa ugani na wasimamizi wa bustani. Kozi 4 zilifanyika katika kipindi cha mwaka uliopita. Washiriki 122 walipata mafunzo.
- Vikundi 27 vya wakulima na bustani kuu 2 zilisaidiwa kuanzisha bustani za vipandikizi kwa kushirikiana na watumishi wa ugani kwenye wilaya 7 (Rombo, Mwanga, Same, Arumeru, Monduli, Karatu na Tarime), kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza miche ya vikonyo. Mpaka sasa miche 18,000 imekwishapandwa katika wilaya hizo.




- Tuliendelea kuitangaza TaCRI na teknolojia zake mpya kwa wadau wa kahawa, hatua ambayo imehamasisha mahitaji ya teknolojia hizo na kuwavutia wageni wengi kufika katika Taasisi yetu.

## VIPAUMBELE MUHIMU 2004—2005

- Kutoa na kusambaza ushauri wa undani kwenye nyanja zote ya uzalishaji wa kahawa na usindikaji wa mwanzo ifikapo katikati ya mwaka 2005 na kuziendeleza kwa takribani vikundi 50 vya wakulima na mashamba 10 makubwa (estates).
- Kuandaa miongozo ya kutoa mafunzo kwenye nyanja zote za uzalishaji na usindikaji wa mwanzo tayari kwa majaribio ifikapo mwishoni mwa 2004.
- Kuanzisha vitalu vinavyosimamiwa na vikundi vya wakulima na mashamba makubwa katika wilaya 5 zaidi.
- Kuendelea kuhamasisha uzalishaji wa miche ya vikonyo na usambazaji wake katika wilaya 12 zilizolengwa.



*Kupandikiza aina mpya ya mbegu kwenye viriba*

- Kuzidi kujenga na kuimarisha mahusiano na watumishi wa ugani, vikundi vya wakulima wadogo na mashamba makubwa kwenye wilaya 5 zaidi kipindi kijacho.
- Kuimarisha kuhusishwa kwa watafiti wa TaCRI na watumishi wa ugani wa wilaya kwenye mbinu shirikishi za utafiti na usambazaji wa teknolojia.
- Kuanzisha mradi wa kuwaandaa wakulima kutumia teknolojia bora (central pulperies) ya usindikaji wa kahawa wa mwanzo ili kuongeza ubora.
- Kuanzisha utafiti utakaobainisha manufaa ya kuhimiza unywaji wa kahawa nchini Tanzania.
- Kuendelea kuratibu ziara zinazoandaliwa kwa wadau.
- Kutangaza na kusambaza teknolojia mpya kwa wadau.
- Kutangaza matokeo ya utafiti kwenye vyombo vya habari.

# IDARA YA USAMBAZAJI TEKNOLOJIA NA MAFUNZO

## UCHUNGUZI KIFANI

*Uzalishaji kwa wingi miche ya vikonyo: Changamoto ya Uzalishaji Kahawa kwa Faida*




*Kichipukizi tayari kwa kupandikiza kwenye kiriba*

Kama ilivyoelezwa kwingineko katika Taarifa hii ya mwaka, moja ya mafanikio muhimu ya TaCRI mapema mwaka 2004 yalikuwa ni kupata "idhini ya awali" ya kutoa na kusambaza aina 5 bora mpya za kahawa chotara. Mafanikio hayo ya kihistoria yametoa changamoto mpya ya kujiandaa kuzalisha kwa wingi na kusambaza aina hizo mpya ili wakulima wa kahawa waweze kuanza kazi ya kuondoa mibuni yao ya zamani na kuweka mipya. Ni mradi mkubwa ambao utahusu kubadilisha mibuni yote ya zamani inayokisiwa kama milioni 200 hivi. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, TaCRI imeamua kuwa na mfumo wa ushirikishwaji ambao unavishirikisha vikundi vya wakulima kwenye uzalishaji na usambazaji wa kasi.

TaCRI hivi sasa ina bustani ya mibuni mama 10,000, ambayo inatarajiwa kila mwaka kutoa vikonyo 500,000 kuanzia 2005. TaCRI ilianza utaratibu wa kuisambaza kwa vikundi vya wakulima, ambao nao wanaanzisha bustani mama zao na utaratibu wa kujizalishia vikonyo kwa gharama nafuu. Kasi itaongezeka kadri vikundi zaidi vya wakulima vitakavyoshirikishwa na wakulima wa mwanzo kuvipatia vikundi vingine vya wakulima miche waliyozalisha. Kwa njia hii wakulima wengi zaidi watajipatia miche kwa haraka zaidi.

Kwa kawaida vikundi vya wakulima huundwa kutokana na shughuli za kuingiza fedha, kwa mfano uzalishaji wa daraja la juu la kahawa ili kupata bei ya juu. Kikundi kimoja cha wakulima kwa wastani kina wanachama kati ya 25 — 30 ambao wanafaidika kutokana na kuchangia pamoja nyenzo na utaalamu. Kwa upande wa kahawa, kama ilivyo kwa kilimo cha mazao mengine, wakulima wanakuwa na nguvu zaidi wakiwa pamoja kuliko kama ni mmoja mmoja. Wanakuwa na uwezo zaidi wa kununua nyenzo na wanakuwa kama "mlango" kati ya Wataalamu wa Masuala ya Kahawa Wilayani (DCSMS) na mkulima mmoja mmoja na njia ya kupitishia teknolojia inayofaa na ya nafuu kwenda chini kwa wakulima.

Ni njia inayotumia gharama vizuri na pia huwezesha upatikanaji wa habari kutoka kwa wakulima, na hivyo kuisaidia TaCRI katika kutathmini ushauri na teknolojia inayotoa ili kuhakikisha kwamba zina kidhi mahitaji ya wadau.



# UCHUNGUZI KIFANI

## MFANO WA MAFANIKIO YA USHIRIKIANO WA MAADILI NA KUPEANA MOYO:
## Shari: Kikundi cha Wakulima Cha Mfano.



*Kikundi cha Shari kikipewa mafunzo na mtaalamu wa TaCRI*

Kikundi cha Shari, wilayani Hai, ni mfano wa jinsi wakulima wanavyoweza kuendesha shughuli kwa pamoja kwa manufaa yao. Kikundi cha Shari kina wanachama 25 ambao kwa pamoja wanamiliki mashine ndogo ya kukoboa kahawa na huuza kahawa yao moja kwa moja mnadani.

Novemba 2003 Kikundi cha Shari kilitokea kuwa kikundi cha kwanza cha wakulima kushiriki katika mpango wa TaCRI wa uzalishaji wa miche kwa kasi. Kikundi hicho kilipewa miche mama 750 ili kiweze kuanzisha bustani mama. Bustani hiyo iko katika hali nzuri na mwezi Novemba mwaka huu wakulima hao wanatarajia kuzalisha miche 30,000 ya kwanza, kwa ajili ya kupanda kwenye mashamba yao binafsi kubadili mibuni ya zamani.

Hadi kufikia mwaka 2005, kikundi hicho kitakuwa kikitoa wastani wa miche 90,000 kila mwaka. Pakiwa na vikundi 300 kama kikundi cha Shari, itawezekana kuzalisha miche milioni 30 kwa mwaka na kuzalisha miche milioni 135 katika kipindi cha miaka mitano tu.


*Uleaji wa miche ya vikonyo kwa ajili ya kusambaza kwa wakulima*


### Mwanzo mzuri na matarajio mema ya baadaye

TaCRI imelenga kusambaza kwa wakulima miche mama ya kwanza 500,000 haraka iwezekanavyo. Mpaka hivi sasa miche 18,000 imekwisha sambazwa kwa vikundi 24 vya wakulima. Kwa kasi hii ya usambazaji, inategemewa kuwa miche mama 100,000 itakuwa imesambazwa ifikapo Desemba 2004. Bodi ya TaCRI imeweka msisitizo mkubwa katika kufufua tasnia ya kahawa, na imeamua kwamba uzalishaji na usambazaji haraka wa miche ni kipaumbele cha kwanza kabisa. Kikundi cha Shari kimedhihirisha kwamba inawezekana!

# IDARA YA UHAKIKA WA RIZIKI NA MAPATO

TaCRI ingali bado inawatafuta watalamu wa kusimamia na kuendesha shughuli za idara hii muhimu hususan mtaalamu wa sosiolojia ya vijijini na mchumi ambao watahitajika kufanya utafiti unaohitajika kuboresha uelewa wa masuala yanayowakabili wakulima wadogo nchini.

Idara imeanzishwa kwa kuwa ni machache mno yanafahamika kuhusu masuala yanayochangia katika kuendeleza na kufanikisha mfumo wa kilimo unaowawezesha wakulima wadogo wa kahawa Tanzania kuishi na kufanya kazi.



*Riziki ya wakulima inaweza kuboreshwa kama watapatiwa aina mpya za mbegu*

VIPAUMBELE VIKUU 2004 — 2005

- Kuajiri wataalamu husika.
- Kufanya utafiti wa kijamii na kiuchumi katika wilaya wakilishi ili kuimarisha uelewa wa masuala yanayowakabili wadau hawa muhimu.
- Kutathmini matokeo ya utafiti na kubainisha ufumbuzi utakaoboresha riziki za wakulima wa kahawa.
- Kutumia matokeo ya utafiti huo kutoa mwongozo kwa idara nyingine za TaCRI kuhakikisha kwamba kazi zote za TaCRI zinaendelea kuwa na maana kwa mahitaji ya wakulima.




Taarifa hii imeandaliwa kwa msaada wa Jumuiya ya Ulaya. Maoni yaliyoelezwa humu ni ya Taasisi Ya Utafiti Wa Kahawa nchini Tanzania na siyo lazima yaakisi maoni ya Jumuiya ya Ulaya.



TaCRI
TAASISI YA UTAFITI WA KAHAWA TANZANIA

**TAASISI YA UTAFITI WA KAHAWA TANZANIA**
**LYAMUNGU**
S.L.P. 3004, Moshi, Tanzania.
Simu / Fax: +255 27 2756773, Email: tacriced@kicheko.com